REF: PPN/12/08

TAARIFA KWA UMMA JUU YA BIASHARA YA MAFUTA KATIKA BAADHI YA MIKOA HAPA NCHINI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA 2008

KWA mujibu wa Agizo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Namba 07-010 la Oktoba 8, mwaka 2007, Mamlaka inaendelea kuchapisha bei za kuagiza baadhi ya mazao ya petroli katika soko la Tanzania.

Sambamba na bei hizo zilizoko katika jedwali Namba 1, pia tumeonyesha orodha ya vituo mbalimblai vya mafuta na bei za mafuta katika vituo hivyo katika mikoa kadhaa hapa nchini katika wiki ya kwanza ya mwezi Septemba katika jedwali Namba 2.

Uchapishaji huu wa bei elekezi si kitu kipya hapa nchini, kwa mfano Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika vipindi tofauti, huchapisha thamani ya fedha katika kipindi husika, lakini thamani halisi ya ubadilishaji wa fedha katika maduka ya kubadilishia fedha hutokana na nguvu ya soko.

Pia ingefaa ieleweke kwamba, kutokana na biashara ya mafuta kuwa huria, EWURA haipangi bei za mazao ya bidhaa zitokanazo na petroli. Lengo la uchapishaji wa bei hizi ni kuwawezesha watumiaji wa bidhaa za mafuta kuwa na picha halisi ya mwelekeo wa bei hapa nchini na katika soko la Dunia

Pia EWURAimelenga kuwapa mwenendo wa bei katika vituo kadhaa hapa nchini ili kuwawezesha kufanya uamuzi wa mahali pa kununua mafuta kulingana na bei ambayo mtumiaji anaridhika nayo. Sambamba na machapisho haya ya bei, EWURA inakuletea pia taarifa za ziada zinazohusiana na mafuta katika soko la hapa nchini, nchi jirani na kwenye soko la dunia.

Jedwali Namba 1: Bei elekezi za mafuta hapa nchini kwa mwezi Septemba 2008)

Maelezo	Kiwango	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Wastani wa Bei soko la Dunia	USD/MT	1,010.05	1,073.70	1,161.80
Bei na Gharama mpaka Dar es Salaam	USD/MT	1,059.51	1,123.25	1,189.03
Gharama za upokeaji	USD/MT	49.08	47.59	50.07
Bei mpaka kutoka bandarini	USD/MT	1,108.59	1,170.84	1,239.10
Bei mpaka kutoka bandarini	TZS/Ltr	956.79	1,144.42	1,142.59
Kodi na Tozo mbali mbali	TZS/Ltr	545.10	520.80	59.10
Faida za na gharama za uendeshaji	TZS/Ltr	83.32	83.00	75.92
Bei ya jumla	TZS/Ltr	1,585.21	1,748.22	1,277.61
Gharama za usambazaji mjini (30 km)	TZS/Ltr	10.00	10.00	10.00
Bei elekezi katika makao makuu ya				

Maelezo Mikoa	Kiwango	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Arusha	TZS/Ltr	1,690.93	1,853.94	1,383.33
Dar es Salaam	TZS/Ltr	1,595.21	1,758.22	1,287.61
Dodoma	TZS/Ltr	1,664.30	1,827.31	1,356.70
Iringa	TZS/Ltr	1,680.21	1,843.22	1,372.61
Kagera	TZS/Ltr	1,852.21	2,015.22	1,544.61
Kigoma	TZS/Ltr	1,852.21	2,015.22	1,544.61
Kilimanjaro	TZS/Ltr	1,673.21	1,836.22	1,365.61
Lindi	TZS/Ltr	1,691.28	1,854.29	1,383.68
Mbeya	TZS/Ltr	1,698.21	1,861.22	1,390.61
Mara	TZS/Ltr	1,835.21	1,998.22	1,527.61
Manyara	TZS/Ltr	1,710.93	1,873.94	1,403.33
Morogoro	TZS/Ltr	1,633.21	1,796.22	1,325.61
Mwanza	TZS/Ltr	1,804.21	1,967.22	1,496.61
Mtwara	TZS/Ltr	1,675.21	1,838.22	1,367.61
Pwani	TZS/Ltr	1,625.21	1,788.22	1,317.61
Rukwa	TZS/Ltr	1,737.65	1,900.66	1,430.05
Ruvuma	TZS/Ltr	1,712.69	1,875.70	1,405.09
Singida	TZS/Ltr	1,682.45	1,845.46	1,374.85
Shinyanga	TZS/Ltr	1,726.58	1,889.59	1,418.98
Tabora	TZS/Ltr	1,726.63	1,889.64	1,419.03
Tanga	TZS/Ltr	1,664.30	1,827.31	1,356.70

Jedwali Namba 2: Bei za mafuta katika baadhi ya vituo vya mafuta Nchini (TZS/Ltr) Kuanzia Wiki ya Kwanza Septemba 2008

MKOA	Petroli	Dizeli	M/Taa
DAR-ES-SALAAM			
New Oryx Kimara Service Station	1,690.00	1,960.00	1,430.00
Total Tabata Service Station	1,675.00	1,980.00	1,400.00
Kobil Nelson Mandela Road Service Station	1,750.00	1,980.00	N/A
Oilcom Kurasini Service Station	1,700.00	1,980.00	1,480.00
BP Mwenge Service Station	1,790.00	2,025.00	N/A
ARUSHA			
BP Arusha Central Service Station	1,885.00	2,120.00	N/A

MKOA	Petroli	Dizeli	M/Taa
Oryx Clock Tower Arusha Service Station	1,818.00	2,135.00	1,575.00
Engen Makumira Service Station	1,700.00	1,960.00	1,550.00
RUVUMA			
Sheckland Filling Station - Mbinga	2,000.00	2,200.00	1,700.00
Jabir Petroleum (T) Ltd - Tunduru	2,000.00	2,200.00	N/A
Kisumapai Filling Station	1,950.00	2,150.00	1,700.00
KIGOMA			
Fuel Master Filling Station	1,900.00	2,100.00	1,700.00
GBP Kigoma Filling Station	2,000.00	2,200.00	1,700.00
World Oil Kigoma Filling Station	1,850.00	2,000.00	1,630.00
KAGERA			
Biharamulo Service Station	1,900.00	2,200.00	1,600.00
Grand Total Service Station	1,880.00	2,160.00	1,650.00
Uganda Road Petrol Station	1,880.00	2,150.00	1,650.00
IRINGA			
Natoil Mafinga Filling Station	1,820.00	2.070.00	1,600.00
Jambek Filling Station	1,750.00	2,100.00	1,550.00
MWANZA			
Oryx Pamba Road Service Station	1,780.00	2,100.00	1,570.00
Mitesh Kenyatta Service Station	1,770.00	2,060.00	1,570.00
GBP Nyamagana Service Station	1,770.00	2,060.00	1,570.00

MALEZO KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA MAFUTA

SOKO LA DUNIA

1.0 Baada ya bei ya mafuta kuweka rekodi ya kupanda kiwango cha juu katikati ya- Julai mwaka huu, bei ya mafuta ghafi imeendelea kushuka kwa kasi kwa zaidi ya dola 31 kwa pipa katika wiki ya pili ya Agosti. Moja ya sababu za kushuka kwa bei ni pamoja na kupungua kwa hali tete ya kijiografia na kisiasa katika baadhi ya nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani. Pia kuimarika kwa thamani ya dola ya Kimarekani dhidi ya fedha nyinginezo imepunguza uwekezaji katika bidhaa za mafuta kama njia ya kuepuka kushuka kwa thamani ya dola. Kutokana na mwenendo huu, uwezekano wa kupata hasara (risks) katika soko la mafuta duniani inaonekana kupungua.

2.0 Bei za wastani kwa wiki za mafuta ghafi kwa aina 14 ambazo huuzwa katika masoko ya eneo hili la Dunia (Brent, Arabian Light, Oman na Murban crude) ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali na mchoro ufuatao.

Mchoro na. 1.0: Mwenendo wa bei ya mafuta ghafi katika Soko la Dunia tangu Januari, 2007 mpaka Agosti, 2008



Jedwali na. 3.0: Bei ya mafuta ghafi katika Soko la Dunia (Juni – Agosti 2008)

	Murban ($/MT)	Arab Light ($/MT)	Brent ($/MT)	Oman ($/MT)
06 Juni, 2008	126.63	120.79	125.47	120.45
13 Juni, 2008	134.47	129.05	134.87	128.29
20 Juni, 2008	136.36	129.66	133.85	129.93
27 Juni, 2008	136.07	130.90	135.98	129.84
04 Julai, 2008	142.68	136.02	142.45	136.72
11 Julai, 2008	143.33	134.55	137.81	137.45
18 Julai, 2008	143.40	134.50	139.34	137.35
25 Julai, 2008	132.57	123.70	129.16	127.56
01 Agosti, 2008	128.62	118.99	125.29	125.46
08 Agosti, 2008	125.12	114.95	120.15	118.74
15 Agosti, 2008	118.39	107.94	114.01	112.35
22 Agosti, 2008	116.09	108.36	110.10	110.22

3.0 Ukilinganisha na bei za mafuta ghafi za mwezi Julai na Agosti, katika kipindi hiki bei imepungua kwa wastani wa asilimia 13.96. Kupungua kwa bei za mafuta ghafi kwa aina kuu nne ambazo huuzwa katika masoko ya eneo hili la Dunia ilikuwa kama ifuatavyo: *Bren,* (14.43%)*, Arab Light* (14.85%), *Murban* (13.13%) *na Omani* (13.41%). Bei za wastani kwa wiki ni kama zilivoonyeshwa katika jedwali namba 3 na mchoro namba 1.

4.0 Katika mwezi Agosti 2008, wastani wa bei ya mafuta kwa aina tatu kuu kabla ya kufikishwa nchini ("FOB") ilikuwa kama ifuatavyo: Petroli, $ 971.36/MT, Dizeli $ 951.72/MT na Mafuta ya taa $ 1,047.89/MT. Bei za wastani kwa mwezi ni kama zinavyoonyeshwa katika jedwali namba 4 na m**choro** namba 2. Kama inavyoonekana katika jedwali namba 4, bei imeshuka katika mwezi Agosti. Kupungua kwa bei ya mafuta katika mwezi Julai na Agosti ni kama ifuatavyo: Petroli, 11.18%; Dizeli, 21.72% na mafuta ya taa, 18.87%.

Jedwali Na. 4: Bei (FOB) za bidhaa za Petroli katika Soko la Dunia (Juni 07–Agosti 2008)

Tarehe	**Petroli**	**Mafuta ya taa**	**Dizeli**
	($/MT)	**($/MT)**	**($/MT)**
Jul-07	719.99	685.60	636.12
Aug-07	664.39	680.91	639.36
Sep-07	698.50	715.51	679.00
Oct-07	710.40	774.89	720.54
Nov-07	801.58	900.18	863.22
Dec-07	769.93	867.23	844.30
Jan-08	803.09	868.23	827.89
Feb-08	859.14	868.29	940.36
Mar-08	881.64	955.72	1,041.65
Apr-08	929.63	1,105.00	1,020.11
May-08	1,057.32	1,134.09	1,150.75
Jun-08	1,128.65	1,156.83	1,189.14
Jul-08	1,093.67	1,291.68	1,215.78
Aug-08	971.36	1,047.89	951.72
Wastani	**863.52**	**932.29**	**908.57**

Mchoro Na. 2: Mwenendo wa Bei za Petroli Katika Soko la Dunia



MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA HAPA NCHINI

5.0 Kati ya mwezi Julai na Agosti 2008, bei ya mafuta katika soko la hapa nchini (Dar es salaam) ikilinganishwa na soko la dunia imepungua kama ifuatavyo. Bei imepungua zaidi katika soko la dunia ikilinganishwa na soko la hapa Dar es salaam. Hii ni kwa sababu taratibu za manunuzi na usafirishaji wa mafuta huchukua kama wiki tatu kukamilika. Hivyo ni matarajio yetu kwamba bei ya mafuta katika soko la hapa nchini itaendelea kushuka katika mwezi Septemba, pamoja na mwenendo wa sasa wa bei katika soko la dunia;

Jedwali Na. 5: Kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia ikilinganiswa na soko la hapa nchini katika mwezi Julai na Agosti 2008

Aina ya Mafuta	Soko la Dunia	Soko la Tanzania
Petrol	11.18%	0.97%
Kerosene	18.87%	0.93%
Diesel	21.72%	0.42%
Average	**17.26%**	**0.77%**

6.0 Bei za mafuta katika soko la ndani hutegemea pia mwenendo wa thamani ya shillingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani. Thamani ya fedha ya Tanzania (Shilingi)

iliongezeka kwa asilimia 1.41 dhidi ya dola ya Marekani katikati ya mwezi Julai na ilipungua katika wiki ya tatu ya mwezi Julai (21 Julai 2008) kama inavyoonyeshwa katika mchoro namba 3 hapo chini. Kwa wastani, shilingi ya Tanzania iliongezeka thamani kwa aslimia 0.37 katika mwezi Julai na ilishuka thamani kwa asilimia 0.05 katika mwezi Agosti..

Mchoro Namba 3: Mabadiliko ya thamani ya shilingi ikilinganiswa na dola ya Marekani



Chanzo: Takwimu za Benki Kuu ya Tanzania

Bei katika nchi jirani

7.0 Mwenendo wa bei ya mafuta katika nchi jirani inafanana na hali ya hapa Tanzania. Bei za mafuta katika baadhi ya nchi jirani na nchi za SADC zimeshuka kwa viwango vinavowiana na vile vya hapa nchini. Jedwali lifuatalo linaonyesha bei katika nchi jirani katika kipindi cha Agosti 2008. Bei za reja reja za mafuta nchini Afrika Kusini Namibia na Msumbiji ziko chini ukilinganisha na za Tanzania, unafuu unaweza kuwa ni kwa sababu nchi hizo hununua mafuta kwa wingi na kwa pamoja.

Jedwali Na. 6: Bei za mafuta hapa nchini na nchi jirani – Agosti 2008

AINA	KENYA (MSA) (USD/LT)	TANZANIA (DSM) (USD/LT)	UGANDA (KLA) (USD/LT)	NAMIBIA (WDH) (USD/LT)	RSA (JBG) (USD/LT)
Petroli	**1.46**	**1.46**	**1.66**	**1.18**	**1.15**
Dizeli	**1.41**	**1.66**	**1.62**	**1.39**	**1.26**
Kerosene		**1.22**		**1.45**	**1.03**

MAJUMUISHO

8.0 Pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kwa wastani wa asilimia 17, ukilinganisha be iza mwezi Julia na Agosti, bei bado ni kubwa na mwenendo wako haujatulia. Kipindi cha baridi kitaanza hivi karibuni katika nchi ambazo hutumia mafuta kwa wingi kwa sababu ya kukabiliana na baridi hali Ambato itaongeza mahitaji ya mafuta na hivyo uwezekano wa kupanda kwa bei ya mafuta.

9.0 EWURA inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe na nchi kama Tanzania ambayo huagiza mafuta ili kulinda uchumi na wateja. Wadau wote wa bidhaa za mafuta hapa nchini wanashauriwa kuchukua hatua mbalimbali ambazo zitawawezesha kupunguza matumizi ya mafuta kila inapowezekana. Hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

9.1 Kununua mafuta katika vituo vya mafuta vyenye bei za chini kwa kulinganisha na bei kwenye vituo vingine katika maeneo yao ili kuchochea ushindani;

9.2 Kuwa na vyanzo mbadala vya nishati kama vile matumizi ya gesi asilia katika magari, katika viwanda na majumbani.

9.3 Kutumia gesi katika uzalishaji wa umeme badala ya mafuta

9.4 Kutumia gesi viwandani badala ya mafuta ya mitambo ambaya huagizwa kutoka nchi za nje. Mpaka sasa jumla ya viwanda 19 hapa Dar es Salaam vimeanza kutumia gesi asilia badaya ya mafuta na au umeme.

9.5 Kutumia gesi (LPG) majumbani badala ya mafuta ya taa, kwa kutoa Mwanza na pia kwa kupikia;

9.6 Kuchangia matumizi ya magari kila inapowezekana; na

9.7 Kwa mtazamo wa muda mrefu, kununua magari yenye injini ndogo. Nchi nyingi hasa za Asia na Ulaya zimeanza kutengeneza na kutumia magari yenye matumizi madogo ya mafuta.

9.8 Mabenki yanahamasishwa kuangalia uwezekano wa kuanzisha mfumo wa kukopesha wateja ili wanunue magari mapya na ambayo yatakuwa yanalipiwa kwa muda mrefu. Mfumo huu utawawezesha watu wengi zaidi kununua magari mapya badala ya yaliyotumika kama ilivyo sasa. Ni ukweli kuwa magari mapya hutumia mafuta kwa kiasi kidogo zaidi kuliko makuu kuu. Nchi nyingine katika ukanda huu zina utaratibu huo na wateja wanapata nafuu hiyo na nchi zinafaidika kwa punguzo la gharama za mafuta na vipuri.

10.0 EWURA itaendelea na utaratibu wa kuchapisha taarifa zinazohusiana na bei za mafuta katika magazeti ili kuwawezesha watumiaji kupata taarifa sahihi za bei na pia kufanya

maamuzi ya mahali pazuri zaidi pa kununua mafuta. Mamlaka pia itakuwa inatoa na kuchapisha kwenye magazeti taarifa zinazohusu ubora wa mafuta yanayouzwa sehemu mbalimbali hapa nchini. Sambamba na hatua hizo, tutaendelea kuchukua na kupima sampuli za mafuta kutoka katika maghala, vituo vya mafuta na yakiwa katika usafirishaji ili kuhakiki ubora na kuchukua hatua kali kwa wahusika inapobainika kuwepo na uuzaji au uwekaji wa mafuta yasiyokidhi viwango. Ni kosa kubwa kuweka au kuuza mafuta yasiyokidhi viwango. EWURA itaendelea kutoa adhabu kali kwa wafanyabiashara pamoja na wasafirishaji wa mafuta watakaokutwa na mafuta yasiyokidhi viwango. Kutokana na juhudi hizi, watumiaji wanapata thamani halisi ya malipo wanayoyafanya kwa kuuziwa mafuta mazuri zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

11.0 EWURA inawakumbusha wafanyabiashara wote wenye vituo vya mafuta kuandika kwenye mbao zinazosomeka vizuri, bei za mafuta yanayouzwa kwenye vituo vyao ili kumuwezesha mnunuzi kuona bei hizo kabla hajafanya maamuzi ya kununua bidhaa za mafuta katika vituo husika. Aidha, vivutio vyovyote vinavyohusiana na biashara hiyo ni budi pia vioneshwe bayana kwenye mbao hizo.

Angalizo: *Ufafanuzi wa maneno mbalimbali yaliyotumika katika taarifa hii unaweza kupatikana katika matangazo yetu ya awali yaliyo katika tovuti ya Mamlaka (www.ewura.com).*

_____

Haruna Masebu
MKURUGENZI MKUU
EWURA